JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

# TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI MEI NA JUNI, 2024

## 1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha mwezi ya Mei, 2024 vipindi vya mvua viliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo ya nchi, hususan katika nusu ya kwanza ya mwezi. Aidha, kutokea kwa kimbunga Hidaya kulisababisha vipindi vya mvua kubwa katika maeneo ya pwani ikiwemo mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani na kupelekea mafuriko na uharibifu wa mali na miundombinu. Katika kipindi cha mwezi Juni, 2024 vipindi vya upepo mkali na baridi vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini ikiashiria kuanza kwa msimu wa Kipupwe, 2024.

### 1.1 Mvua kubwa kwa mwezi Mei, 2024


Katika kipindi cha mwezi Mei, 2024 vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan nusu ya kwanza ya mwezi. Kutokea kwa kimbunga Hidaya mnamo tarehe 30 Aprili, 2024 hadi 04 Mei, 2024 katika eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi kulisababisha vipindi vya mvua kubwa na upepo mkali katika maeneo ya ukanda wa pwani na kupekelea mafuriko na uharibifu mkubwa wa mali na miundombinu pamoja na vifo. Kimbunga Hidaya kilitua katika kisiwa cha Mafia tarehe 4 Mei, 2024. Mnamo tarehe 4 kituo cha Kilwa (kilichopo mkoa wa Lindi) kiliripoti kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 316.6 ndani ya saa 24. Kiwango hiki ni sawa na asilimia 327 ya wastani wa muda mrefu wa mvua kwa mwezi Mei kwa kituo cha Kilwa.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*728G _ 01/2023*




**Kielelezo 1:** Vituo vilivyoripoti viwango vya mvua kubwa kiasi cha milimita 50 au zaidi ndani ya saa 24 kwa mwezi Mei, 2024.


Athari mbalimbali ziliripotiwa katika baadhi ya mikoa ikiwemo mikoa ya Pwani, Morogoro, Lindi na Mtwara baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha mafuriko, uharibifu mkubwa wa mali na miundombinu pamoja na kuathiri shughuli za kiuchumi.




**Kielelezo 2**. Kipande cha barabara kikiwa kimekatika kutokana na mafuriko yaliyosababishwa na Kimbunga Hidaya katika eneo la Somanga, Lindi (Chanzo: *Communications department Ministry of Public Works Tanzania*)

### 1.2 Hali joto kwa mwezi Mei, 2024

Katika kipindi cha mwezi Mei 2024, hali ya joto iliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchin, hata hivyo hakukuwa na joto kali zaidi vilivyoripotiwa katika kipindi hiki. Aidha, vipindi vya baridi kali vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi, hususan mikoa ya Mbeya na Njombe. Kielelezo 3 kinaonyesha viwango vya joto la chini vilianza kushuka kuanzia wiki ya pili kuelekea mwishoni mwa mwezi, na kiwango cha chini zaidi cha joto cha nyuzi joto 7 kiliripotiwa katika kituo cha Uyole mnamo tarehe 30 Mei, 2024. Katika mwezi huu kituo cha Uyole (mkoa wa Mbeya) kiliripoti viwango vya nyuzi joto chini ya 10 °C kwa muda wa siku 13 ikifuatiwa na kituo cha Igeri siku 9.




**Kielelzo 3.** Viwango vya joto la chini kituo cha Uyole na Igeri katika mwezi Mei, 2024.

### 1.3 Upepo Mkali kwa mwezi Mei, 2024

Katika kipindi cha mwezi Mei, 2024 vipindi vya upepo mkali unaofika na kuzidi kilomita 40 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini. Kutokana na uwepo kimbunga Hidaya mwanzoni mwa mwezi kulisababisha vipindi vya upepo mkali na kuathiri maeneo ya ukanda wa pwani ikiwemo mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba. Nguvu ya upepo ilisababisha athari mbalimbali katika maeneo hayo.


### 1.4 Mvua kubwa kwa mwezi Juni, 2024

Katika kipindi cha mwezi Juni, 2024 vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo machache ya nchi, hususan mwambao wa pwani na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika maeneo ya pwani ya kaskazini mnamo tarehe 18 na 19 Juni, 2024. Mnamo tarehe 19 Juni, 2024

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

kituo cha Matangatuani kilichopo kisiwa cha Pemba kiliripoti kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 109.0 kwa saa 24. Vituo vilivyoripoti mvua ya milimita 50 au zaidi ni kama inavyoonekana katika kielelezo 4.




**Kielelezo 4:** Viwango vya mvua kubwa kwa mwezi Juni, 2024

### 1.5 Hali joto kwa mwezi Juni, 2024


Kwa kuzingatia hali ya hewa ya muda mrefu (Klimatolojia) kwa mwezi Juni, hakuna hali ya joto kali iliyojitokeza katika kipindi hiki. Hata hivyo, viwango vidogo vya joto la chini vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan nyanda za juu kusini magharibi. Kiwango kidogo zaidi cha joto la chini kilichorekodiwa katika kituo cha Uyole mkoani Mbeya kilikuwa ni nyuzi joto 4.8 °C mnamo tarehe 15 Juni, 2024. Aidha, katika kipindi hiki vituo vya Uyole na Igeri viliripoti viwango vya joto chini ya nyuzi joto 10 °C kwa siku 25 kwa kila kituo.Jedwali namba 1 linaonyesha idadi ya siku ambazo kituo kimerekodi kiwango cha joto la chini cha nyuzi joto 10 °C au chini ya nyuzi joto 10 °C.

Jedwali 1. Viwango vidogo vya joto la chini vilivyojitokeza mwezi Juni, 2023

| Kata | Kituo | Idadi ya Siku | Joto la Chini ($^0$C) |
|---|---|---|---|
| **Southwestern highlands** | Uyole | 25 | ≤ 10 °C |
| | Igeri | 25 | ≤ 10 °C |
| | Mbozi | 4 | ≤ 10 °C |
| | Sumbawanga | 9 | ≤ 10 °C |

Kielelezo cha 5 kinaonesha viwango vya joto la chini kwa kila siku kwa mwezi Juni, 2024 kwa vituo vya Uyole na Igeri. Kwa ujumla, hali ya baridi kali ilianza kujitokeza katika wiki ya kwanza mwezi Juni. Hata hivyo, viwango vya joto la chini vinaonesha hali

ya baridi zaidi ilijitokeza katika maeneo ya Uyole kati ya wiki ya pili na ya tatu ambapo kiwango cha joto la chini kilipungua zaidi  hadi chini ya nyuzi joto 5 °C.




**Kielelzo 5.** Viwango vya joto la chini kituo cha Uyole na Igeri katika mwezi June, 2024.

**1.6 Upepo Mkali kwa mwezi Juni, 2024**

Katika kipindi cha mwezi Juni, 2024 vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini ikiwemo ukanda wa pwani (Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba), pamoja na maziwa makuu. Hii inaashiria kuanza kwa msimu wa Kipupwe, 2024 ambao hutawaliwa na upepo mkali wa kusi. Nguvu ya upepo mkali ilisababisha athari mbalimbali katika maeneo hayo ikiwemo kusambaa kwa vumbi, kupeperushwa kwa takataka na kusababisha kupungua kwa uono. Maeneo machache ya mwambao wa pwani ya bahari yalipatwa na vipindi vya mawimbi makubwa na kuathiri baadhi ya shughuli zinazofanyika baharini sambamba na kuhatarisha jamii zinazofanya shughuli mbalimbali katika maeneo ya mwambao..

*Matukio haya ya hali mbaya ya hewa yanaonesha ongezeko la changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na umuhimu wa kutekeleza mikakati thabiti ya kukabiliana mabadiliko hayo ili kulinda jamii na mazingira*.

*Imetolewa: tarehe 10 Julai, 2024*
**Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**


*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz